**RISALA YA UTII YA WANANCHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MH: DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, KATIKA MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU TAREHE 06/06/2018**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Rais**, Sisi Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea tunayo furaha na heshima kubwa kuukaribisha Mwenge wa Uhuru pamoja na wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa na Kimkoa wakiongozwa na **Ndugu Charles Fransis Kabeho,** leo tarehe 06/06/2018 hapa Wilayani kwetu Songea. Mwenge wa Uhuru tunaupokea na kuukimbiza kwa mara nyingine ukiwa unatimiza miaka hamsini na nne (54) tangu uanze kukimbizwa hapa nchini na miaka ishirini na tano (25) tangu Mbio za Mwenge wa Uhuru zirejeshwe chini ya utaratibu wa usimamizi wa Serikali.

**Mheshimiwa Rais**, Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea tunatambua umuhimu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kuwa ni chachu ya kuleta maendeleo, kurejesha matumaini pale pasipo na matumaini, kuleta upendo mahali palipo na chuki, na heshima palipojaa dharau. Aidha unasaidia kuongeza kasi ya shughuli za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Hivyo wote tuko bega kwa bega katika kuendeleza azma hii na hivyo kujiletea maendeleo yetu na hatimaye kuondokana na umaskini kwa ujumla.

## 2.0 HALI YA HALMASHAURI YA WILAYA

**Mheshimiwa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea, inapakana na Jamhuri ya watu wa Msumbiji upande wa Kusini Mashariki, Kusini Magharibi tunapakana Nyasa, upande wa Mashariki tunapakana na Namtumbo, Manispaa ya Songea kwa upande wa Kaskazini Mashariki, Madaba kwa upande wa kaskazini na Mbinga Vijijini na Halmashauri ya Mji Mbinga kwa upande wa Magharibi. Halmashauri ya Wilaya ya Songea ni moja ya Halmashauri tatu za Wilaya ya Songea pia miongoni mwa Halmashauri nane za Mkoa wa Ruvuma. Halmashauri ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 10,052.96

**Mheshimiwa Rais**, Kutokana na Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2012 Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilikuwa na wakazi 173,821 (Wanawake 87,273 Wanaume 86,548). Kwa sasa Halmashauri inakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi 141,427 kati ya hao wanawake 71,008 na wanaume ni 70,419 pia Halmashauri ina kaya 31,428. Halmashauri ina sifa ya kuwa na mvua za kutosha na joto la wastani. Mvua zinakadiriwa kunyesha kati ya mm 1000 na mm 1500 ambazo ni nzuri kwa kilimo. Joto hubadilika kutokana na nyakati ambapo linafikia wastani wa $20^{o}$C- 25 $^{o}$C wakati wa joto kali na kati ya $15^{0}$C na $17^{0}$C wakati wa usiku**.** Mvua huanza kunyesha mwezi Novemba na kumalizika Mei kila mwaka.

.

## 3.0 MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018

**Mheshimiwa Rais,** Sisi wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea tumeendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa Taifa tukiwa tunajiandaa kuupokea Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2018. Tumeshiriki katika kutekeleza miradi mbalimbali na baadhi yake imepitiwa na Mwenge wa Uhuru, Miradi hiyo ni ujenzi wa Madarasa 4, matundu ya vyoo 6, ujenzi wa nyumba ya mwalimu, Shamba la kahawa, Bustani ya umwagiliaji kwa matone JKT Mlale, uzinduzi wa mafunzo ya vishikwambi (Tablets) Shule ya Msingi Mbinga Mharule, ujenzi wa Maabara Shule ya Sekondari Mkombozi, Viwanda vidogo vidogo Kijiji cha Nakahegwa, ukaguzi wa zahanati kijiji cha Lipokela,

Tumeshirikiana pia katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria, Madawa ya kulevya na Rushwa na uimarishaji wa vikundi vya ujasiliamali vya akina mama na vijana.

## 4.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA UJUMBE WA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018, "ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA WEKEZA SASA"

**Mheshimiwa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea inaendelea kutekeleza mikakati shirikishi ya uendeshaji na usimamizi wa Elimu, Halmashauri yetu ina Shule za Msingi 69 za Serikali na 2 za binafsi na Madarasa ya Awali 71 ambayo yapo katika kila Shule ya Msingi. Shule hizi zina darasa la Awali - VII na jumla ya wanafunzi 31,482 ikiwa wavulana 16,036 wasichana 15,446. Ongezeko hilo kubwa limetokana na mwitikio wa wazazi kuandikisha watoto wao kwa darasa la awali na la kwanza kufuatia agizo lako Mheshimiwa Rais la Elimu bila malipo.

Aidha Wilaya ililenga kuandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza na Awali kwa Mwaka 2017/2018 kama ifuatavyo:- Darasa la Awali Maoteo, wavulana 2,239 na wasichana 2,062 jumla 4301 uandikishaji wavulana 2,215 wasichana 2050 jumla 4,265 sawa 99% na darasa la kwanza Maoteo wavulana 2,011 wasichana 1,894 jumla 3905 uandikishaji wavulana 2,339 wasichana 1961 jumla 4,300 sawa 110%. Kupitia Mpango wa Elimu bila malipo Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa mwaka 2016/2017 imepokea jumla ya Tshs. 156,309,936.40. Kwa mwaka 2017/2018 Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs. 285,711,120/=. Upatikanaji wa fedha hizi umeboresha miundombinu mbalimbali ya Shule hivyo kufanya kazi ya ufundishaji kuwa rahisi kwa Walimu.

**Mheshimiwa Rais,** Hali ya madawati kwa sasa inaendelea kuimarika ukilinganisha na mwitikio wa wazazi wa kuandikisha watoto wao wa darasa la Awali na Shule ya Msingi. Hivyo mahitaji ya madawati ni 10,494, yaliyopo ni 9,804, na upungufu ni madawati 690. Jitihada za kukabiliana na upungufu zinafanyika kwa kutenga fedha za Halmashauri. Wilaya Songea imeendelea kutekeleza Miradi ya Lipa kulingana na matokeo (P4R) kwa mwaka wa 2016/2017 Jumla fedha kiasi cha Tshs. 176,000,000/= (Milioni mia moja sabini na sita tu) zilipatikana ikiwa kwa ajili ya ujenzi vyumba vya Madarasa 6, matundu ya vyoo 20, ukarabati wa miundombinu kwa mchanganuo ufuatao, shule ya Msingi Kivukoni Tsh. 141,000,000/= na AboudJumbe Tshs. 31,000,000/= Aidha, kila shule ilitengewa Tshs. 2,000,000/= kwa ajili ya ufuatiliaji.

**Mheshimiwa Rais,** Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs. 177,200,000 (milioni mia moja sabini na saba mia mbili elfu tu) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 8 na matundu ya vyoo 12 katika Shule ya Msingi mbili (2). Aidha miradi katika shule zote mbili ilikamilika na kukabidhiwa kwa kamati za shule. Halmashauri imepokea fedha za motisha za P4R (Msingi na Sekondari) Tshs. 283,559,039.9 ambazo zinatumika kadiri ya mwongozo ikiwa ni ukusanyaji wa takwimu, usimamizi wa elimu, ufuatiliaji na tathmini, upangaji wa ikama ya walimu wa shule za msingi, ujenzi wa madarasa mapya na ukamilishaji wa ujenzi wa maabara za sayansi.

**Mheshimiwa Rais,** Wilaya ina jumla ya Shule za Sekondari 21, kati ya hizo 16 zinamilikiwa na serikali na 5 zinamilikiwa na mtu binafsi. Jumla ya wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali ni 5073 ikiwa Wavulana ni 2314 na Wasichana ni 2759 na wale wa Shule binafsi ni Wavulana 259 na Wasichana 996. Wilaya ya Songea ina Shule mbili (2) za Serikali za Kidato cha Tano na Sita ambazo zina Wanafunzi 569 wakiwemo wavulana 215 na wasichana 354. Pia kuna shule moja (1) ya binafsi yenye wanafunzi wa kidato cha tano na sita ambayo ina jumla ya wanafunzi wa kike 73. Mahitaji ya meza ni 5073, viti 5073, meza zilizopo **3,946,** viti vilivyopo **3,329,** upungufu wa meza**1,127,** upungufu wa viti **1,744.** Halmashauri ya Wilaya ya Songea imepokea fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi katika Shule za sekondari kupitia:-

Mpango wa MMES II,  Shule 3 zilinufaika na mpango huo kwa kupokea jumla ya Tshs. **384,641,084.00** kwa kipindi cha 2016/2017. Shule hizo ni:- Matimira sekondari ambayo ilipokea jumla ya **Tshs. 188,360,508.00** Kwa ajili ya ukarabati wa vyumba 10 vya madarasa, ujenzi wa matundu mawili ya vyoo na uwekaji umeme jua,  Lupunga Sekondari ilipokea jumla ya **Tshs. 22,803,201.00** kwa ajili ya ujenzi wa vyoo matundu 8 na Liganga Sekondari ilipokea **Tshs 173,477,375.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1 (moja) ya walimu na ujenzi wa vyoo matundu nane.

Mpango wa Lipa kulingana na Matokeo ya (P4R) Shule moja ya sekondari hadi sasa imenufaika na mpango huu kwa kupokea jumla ya **Tshs. 160,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Hostel na ukarabati wa miundombinu ya shule ya Sekondari Barabarani. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo:-  Ujenzi wa Hostel **Tshs 150,000,000.00** na Ukarabati wa miundombinu ya shule **Tshs 10,000,000.00**. Aidhaa Wilaya ya Songea inatekeleza mradi wa ujenzi wa mabweni 2 ya kulaza wanafunzi 160 katika Shule ya Sekondari Barabarani kwa kupitia fedha za P4R. Kupitia miradi ya MMES II na P4R Wilaya, imepokea jumla ya **Tshs. 544,641,084.00**,  kwa shule za sekondari.

## 5.0 MAPAMBANO DHIDI YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Rais,** Halmashauri ya Wilaya imeendelea  na mapambano dhidi ya madawa ya kulevya ambapo elimu imetolewa kuhusu madawa ya kulevya  na takwimu zinaonekana makosa na kesi katika mahakama zimepungua kwa kiasi kikubwa ambapo kwa mwaka  2017 kesi za madawa ya kulevya zilikuwa 109 na zimepungua kwa kesi 17 na mwaka 2018 kuna  jumla ya kesi 92 tu.

## 6.0 MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

**Mheshimiwa Rais,** Jitihada katika kuhamasisha wananchi kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa yamefanywa chini ya Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa (TAKUKURU) kwa kuhamasisha wananchi kufichua kitendo vya rushwa kwenye maeneo yao, hii imepelekea wananchi kutoa raatifa zipatazo 33 za vitendo vya rushwa, wananchi wapatao 989, walielimishwa kupitia njia mbalimbali kama Semina, Mkutano ya hadhara, Makongamano, Warsha, Vilabu vya wapinga rushwa mashuleni na vyuoni, pia machapisho mbalimbali 167 yalipelekwa kwa wananchi.  Vyombo vya habari vimeshiriki kikamilifu kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye mapambano dhidi ya rushwa hasa Radio za Umma na Binafsi.  Wananchi wameendelea kushirikishwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, hii imewezesha wananchi kufichua vitendo vya matumizi mabaya ya fedha za umma kwenye miradi, ushiriki wao kwenye miradi umewezesha miradi zaidi 4 kuchunguzwa kwa matumizi mabaya ya fedha za umma, zoezo la ukaguzi wa miradi mingine linaendelea

## 7.0 SEKTA YA MAJI

**Mheshimiwa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea  inatekeleza miradi mitano.  Mradi wa maji mtiririko Luyelela utahudumia Jumla ya vijiji saba (7) utakapokamilika kwa gharama ya Tshs. 6,369,261,390.00. Hadi sasa jumla ya TShs. 583,506,696 zimeshalipwa kwa mkandarasi.  Ujenzi wa mradi wa maji mtiririko Liula Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua za mwisho kukamilika. Mradi huu ulikadiriwa kugharimu kiasi chaTshs. 1,005,798,776.13 na mpaka sasa Tshs. 839,794,077 tayari zimeshalipwa kwamkandarasi. Ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Lipaya – Mpitimbi ambao utahudumia  vijiji vitatu na utakapokamilika utagharimu jumla ya Tshs. 1,400,000,000.00 umeanza kutekelezwa na Mapema mwaka 2017 Halmashauri ilipata msaada wa Shilingi 42,000,000 kutoka Ubalozi wa China nchini Tanzania kusaidia mradi huu.  Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa msaada wa Wamisionari Wabenediktini wa Hanga ilifanikiwa kujenga na kufunga pampu visima 37. Aidha, wanatekeleza mradi mkubwa wa maji mtiririko vijiji vya Muhukuru Lilahi na Barabarani. Kwa sasa Halmashauri ipo kwenye maandalizi ya ujenzi wa miradi mipya ya maji katika vijiji 13 ambapo inakusudia kujenga miradi ya maji mtiririko katika vijiji 8, uchimbaji wa visima virefu 26 katika vijiji vitano .Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Aprili 2018 Halmashauri imepokea jumla ya Tshs. 651, 893,709.60 kwa ajili ya shughuli za maji katika Halmashauri. Katika kipindi cha kuanzia Julai

2017 hadi Aprili 2018 Halmashauri imepokea jumla ya Tshs. 593,905,347- kwa ajili ya shughuli za maji katika Halmashauri katika mchanganuo ufuatao:- Tshs. 537,905,346.60 - Malipo ya Wakandarasi wa Luyeleha, Ukarabati wa vituo na miundombinu ya kuchotea maji, Tshs. 30,000,000.00 - Kampeni ya afya na Usafi wa mazingira na Tshs. 26,000,000.00 - Uendeshaji wa ofisi, usimamizi na ufuatiliaji

## 8.0 SEKTA YA UJENZI

**Mheshimiwa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina Mtandao wa barabara ulioingizwa kwenye mfumo wenye Jumla ya km 1005.6 Jumla ya km. 13.97 ni barabara za lami, km 44.92 ni za changarawe na zinapitika vizuri, km.338.41 ni za udongo hali yake ni ya wastani zinapitika kwa shida wakti wa masika, km 581.3 ni za udongo ambazo zinapitika kwa shida na kwa kipindi cha masika hazipitiki kutokana na uharibifu wa maji ya mvua. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilitengewa jumla ya Tsh.1,022,900,000 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zenye urefu wa km 122 ambazo ni sawa na asilimia 12.13% ya mtandao wote wa barabara.Hadi sasa tumepokea jumla ya Tsh.664,375,682.54.

## 7.0 SEKTA YA AFYA

**Mheshimiwa Rais,** Wilaya ina jumla ya vituo vya kutolea huduma 33, ambavyo kati ya hivyo Hospitali ni 1, kituo cha Afya ni 1, na Zahanati ni 31, ambapo Hospitali inamilikiwa na shirika la Dini, kituo cha afya kinamilikiwa na Serikali na zahanati 21 zinamilikiwa na serikali, zahanati 9 zinamilikiwa na Mashirika ya dini na 1 inamilikiwa na jeshi (JKT Mlale). Wilaya imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa chanjo mbali mbali za watoto na mama wajawazito kama vile chanjo za kukinga kifua kikuu, ugonjwa wa kupooza, kukinga magojwa ya pepopunda, donda koo, homa ya ini na kifaduro, vichomi, uti wa mgongo, na Surua. Kuanzia mwanzoni mwa mwezi Januari 2017 hadi sasa hatuna upungufu wa chanjo kwa Wilaya ya Songea. Malengo nikufikia asilimia 95 ya watoto wote kuwa wamepata chanjo, kwa sasa tupo asilimia107. Kiwango cha utapiamlo mkali ni **asilimia** 0.03 na utapia mlo usio mkali ni **asilimia** 0.1.

Pamoja na changamoto mbalimbali za sekta ya Afya, Wilaya imefanikiwa kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka asilimia 5.2 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 3 mwaka 2017/2018. Vifo vya akinamama wajawazito (martenal Mortarity) vimepungua kutoka **84/100,000** kwa mwaka 2015 hadi kufikia **17/100,000** mwaka 2017. Bado jitihada za kupunguza vifo hivyo vya akinamama zinaendelea ikiwa ni pamoja na kuanzisha huduma za upasuaji. Halmashauri ya wilaya ya Songea imekuwa ikitekeleza shughuli za Mfuko wa wa Afya ya jamii (CHF) tangu mwaka 1998 ambapo shughuli za kuhamasisha jamii kujiunga na CHF zimefanyika katika kata zote 16. Hadi kufikia Disemba, 2017 uchangiaji ni asilimia 21. Pia utoaji wa vitambulisho bure kwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka 60 umefanyika kwa wazee 8841, sawa na asilimia 68 kati ya wazee 13,060 (me 6,206, ke 6,854) wanaotarajiwa kufikiwa hadi 2018 katika kata zote 16. Aidha, kwa sasa wazee wote ambao hawajafikiwa na kupatiwa vitambulisho maalumu vya matibabu, watatambuliwa kwa vitambulisho vya kupigia kura.

## 9.0 MAZINGIRA

**Mheshimiwa Rais**, Hali ya usafi katika vijiji vyote 56 inaridhisha kwani zoezi la usafi wa mazingira limekuwa endelevu kwa kufanya usafi wa mazingira kila jumamosi ya mwisho wa mwezi, ikiwa ni utekelezaji wa agizo lako Mheshimiwa Rais. Hali ya ujenzi wa vyoo Vijijini kwa mwaka 2017 imefikia asilimia 86 kwa vyoo vya kawaida na asilimia 48 vyoo bora. Halmashauri ya Wilaya ya Songea imepokea dawa za kuulia Wadudu wa Mbu `Larvicide` kutoka Kibaha, lita 820. Madimbwi 25 yaliyotambuliwa yenye ukubwa wa mita za mraba 48,846 yenye mazalio ya kudumu ya Mbu yalipuliziwa dawa.

## 10.0 KILIMO

**Mheshimiwa Rais,** Hali ya zana za kilimo katika Wilaya yetu imeendelea kuwa tatizo kwa sababu bado wakulima wengi wanatumia jembe la mkono. Aina ya zana za kilimo zilizopo ni pamoja na trekta kubwa mahitaji 120, zilizopo 78 na pungufu 42.Trekta ndogo ndogo (Power tillers) Mahitaji 100, zilizopo 76, pungufu 24. Mashine za kuvunia mpunga (combine harvester) Mahitaji 2, zilizopo 2 pungufu hakuna. Mashine ya kupura mpunga mahitaji 2, zilizopo 2, pungufu hakuna, mtambo wa kusindika mpunga mahitaji 1, zilizopo 1, pungufu hakuna. Eneo linalofaa kwa Kilimo cha umwagiliaji ni Hekta 17,000, kati ya hizo eneo linalolimwa lenye miundo mbinu iliyojengewa ni Hekta 1,340 na eneo linalolimwa ambalo halina miundo mbinu iliyojengewa ni Hekta12,160. Hivyo kufanya jumla ya eneo linalolimwa kwa umwagiliaji kuwa Hekta 13,500. Hadi kufikia sasa kuna jumla ya skimu 6 za umwagiliaji ambazo zimejengewa miundo mbinu kati ya skimu 26 zilizopo. Pia shamba la mwekezaji lina Hekta 1,025 za kahawa zenye miundo mbinu ya umwagiliaji iliyojengewa na hivyo kufanya jumla ya eneo lililoendelezwa kuwa Hekta 2,365. Katika skimu zilizojengewa miundo mbinu na kuendelezwa uzalishaji wake ni wastani wa gunia 50 kwa Hekta Wakati katika skimu ambazo hazijajengewa miundombinu uzalishaji wake ni wastani wa gunia 15 kwa Hekta. Hata hivyo skimu hizi hazijakamilika ujenzi wa miundo mbinu kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kuendeleza skimu hizo.

## 11.0 MIFUGO

**Mheshimiwa Rais,** Wilaya ina jumla ya ng’ombe 23,000 kati ya hao ng’ombe 20,662 ni wa asili na ng’ombe 2,338 ni wa maziwa, aidha kuna nguruwe 48,894, Mbuzi 37,657, kondoo 3,532 na kuku 294,522, mbwa 9,113 paka 753, na bata 3,819. Serikali imekuwa ikiboresha sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundo mbinu ya kutolea huduma za mifugo. Miundombinu iliyoboreshwa ni pamoja na:- ujenzi wa machinjio 1, Majosho 14 kati ya hayo majosho 7 yanafanya kazi na Majosho 7 bado hayafanyi kazi. Halmashauri inakadiriwa kuwa na eneo la hekta 119, 687 zinazofaa kwa shughuli za ufugaji, aidha ni hekta 33,771 tu ndio zimetengwa na kutumika kwa ajili ya shughuli za ufugaji. Aidha Wilaya imetoa chanjo kwa wanyama kama ifuatavyo; kuku **215,000** kati ya **294,522,** dhidi ya ugonjwa wa kideri ambayo ni sawa na **72.9%** na mbwa **7,602** kati ya **9,113** dhidi ya ugonjwa wa Kichaa cha mbwa sawa na **83.42%.** Halmashauri ya Wilaya Songea inaendelea kutekeleza Sheria Na **12** ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliajia wa Mifugo ya Mwaka **2010** kwa kupiga chapa mifugo (ng’ombe) katika Wilaya. Mpaka sasa jumla ya ng’ombe **14,922** wamepigwa chapa sawa na **87.09%** kati ya ng’ombe **17,250** wenye umri wa kupiga chapa.

## 12.0 UVUVI

**Mheshimiwa Rais,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina mialo miwili (Landing station) iliyo kandokando ya mto Ruvuma katika vijiji vya Nambendo na Magwamila. Hadi sasa kuna wavuvi (wadogo wadogo) wapatao 60. Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina wafugaji wa samaki 1,327 wenye jumla ya mabwawa 3,227 yakiwemo mabwawa ya asili 24. Katika kudhibiti uvuvi haramu Halmashauri ya Wilaya ya Songea inatekeleza mpango kazi katika vijiji vya Nambendo na Magwamila wa kuhakikisha elimu na usimamizi bora wa rasilimali za uvuvi unafanyika kwa wavuvi na wananchi wote wanaojishughulisha na uvuvi katika maeneo ya Mialo.

## 13.0 UKUSANYAJI NA USIMAMIZI WA MAPATO

**Mheshimiwa Rais**, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilipangiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs.26,820,213,440**. Hadi kufikia tarehe 30.06.2017 ilikusanya na kupokea jumla ya **Tshs.20,650,054,623.66** sawa na **76.99**% ya makisio ya mwaka na kutumia

**Tshs.21,176,347,429.93** sawa na **78.95%** ya makisio ya mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wilaya ilikisia kukusanya mapato ya ndani jumla ya **Tshs. 1,458,637,000** hadi kufikia 30.06.2017 tulifanikiwa kukusanya **Tshs. 901,264,669.20** sawa na 61.78% ya bajeti ya mapato ya ndani. Halmashauri ya Wilaya ya Songea, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wilaya ya Songea ilipangiwa kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 31,193,200,559** kati ya fedha hizo **Tshs.1,066,130,000** ni makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani, **Tshs.16,096,281,000** Mishahara, **Tshs. 903,031,601** Matumizi ya kawaida (OC) na **Tshs. 10,930,941,959.00** miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi machi, 2018 Halmashauri imekusanya jumla ya **Tshs.452,824,299.04** sawa na 42.47% ya makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani na **Tshs.9,079,065,500** mishahara sawa na 56.40%, matumizi ya kawaida **Tshs.601,941,400.00** sawa na **66.66%** na **Tshs. 2,997,213,584** mapokezi ya fedha za miradi kwa mwaka 2017/2018 sawa na **22.83%**. Halmashauri ya Wilaya ya Songea, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wilaya yetu inaendelea kukusanya na kudhibiti ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutumia mfumo wa kielekroniki wa LGRCIS, kwani hadi sasa tuna mashine za ukusanyaji mapato (POS) 45. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imepanga kuongeza mashine 21 ili kukidhi uhitaji wa kuwa na mashine kwa kila kijijini na vizuizi vyote vya kukusanyia mapato.

## 14.0 MICHANGO YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017

**Mheshimiwa Rais**, Kama ilivyo kawaida Serikali na wananchi wamekuwa na jukumu la kuchangia michango ya fedha, mali na nguvu kwa madhumuni ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na shughuli za Mwenge wa Uhuru kwa ujumla. Kwa mwaka huu 2017 Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru alifungua miradi mitatu (3) yenye thamani ya **Sh. 226,658,835.00** na kuweka mawe ya msingi miradi miwili (2) yenye thamani ya **Sh. 667,540,000.00** na Shughuli za uzalishaji mali zenye thamani ya **Sh.21,000,000.00.** Jumla ya miradi yote imegharimu kiasi cha **Sh 915,198,835.00** Aidha wananchi wamechangia **Sh. 29,674,100.00**, kwa ajili ya Mwenge wa Uhuru 2017 na fedha hizi zimetumika katika miradi ya maendeleo.

## 15. 0 MICHANGO YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2018

**Mheshimiwa Rais**, Serikali na wananchi wamekuwa na jukumu la kuchangia michango ya fedha, mali na nguvu kwa madhumuni ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na shughuli za Mwenge wa Uhuru kwa ujumla. Mwaka 2018 Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru atafungua miradi miwili (2) yenye thamani ya **Sh. 117,715,000.00,** kuweka mawe ya msingi miradi miwili (2) yenye thamani ya **Sh. 838,755,000.00,** Miradi mitatu (3) ya kuzinduliwa yenye thamani ya **Sh. 533,435,000.00** na Miradi ya miwili (2) kukaguliwa yenye thamani ya **Sh.126,470,080.00.** Jumla ya miradi yote imegharimu kiasi cha **Sh 1,616,375,080.00.** Aidha wananchi wamechangia **Sh. 41,459,100.00**, kwa ajili ya Mwenge wa Uhuru 2018 na fedha hizi zimetumika katika miradi ya maendeleo.

***MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA***
***MUNGU UBARIKI MKOA WETU WA RUVUMA***
***MUNGU WABARIKI WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU 2018***
***NI SISI WANANCHI WA HALMASHAURI YA WILAYA SONGEA***

**MWENGE WA UHURU OYEEEEEEEEEEEEEEEEE!!!!!!!!!!!!!!!!**
**POLOLET KAMANDO MGEMA**
**MKUU WA WILAYA**
**SONGEA**